# HALMASHAURI YA MJI WA KASULU

**ZABUNI NA: LGA/169/2022/2023/NC/01/L/03**

Kwa ajili ya:

**TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI WA MGAHAWA WA HALMASHAURI (CANTEEN)**

**Tarehe 15 Juni, 2022**

Halmashauri ya Mji KASULU inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuendesha mgahawa wa Halmashauri uliopo makao makuu ya Halmashauri ya mji wa Kasulu.

Unakaribishwa kuleta kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na bei kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya II.

Kotesheni zote ziwe na nakala halisi (original) nakala moja zinazofanana,zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na**. LGA/169/2022/2023/NC/01/L/02** Ni lazima kupelekwa kwa katibu wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Mji Kasulu,S.L.P 475 Kasulu ofisi ya kitengo cha ununuzi Ugavi,chumba Na.40 ghorofa ya pili.

Siku ya mwisho ya kuwasilisha kotesheni ni **Jumatatu tarehe 20 JUNI, 2022** kabla ya saa 4.30 asubuhi. Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya ufunguzi, mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakao kuwa wamehudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa mikutano Halmashauri ya Mji Kasulu,S. L. P 475 Kasulu.

Kotesheni zitakazochelewa,sehemu, kotesheni za kielektronic, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

| Na | Maelezo ya Zabuni | Kotesheni Namba |
|---|---|---|
| i | **UENDESHAJI WA MGAHAWA WA HALMASHAURI YA MJI KASULU.** | **LGA/169/2022/2023/NC/01/L/03** |

**Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;-**

I. Mwombaji ni lazima awe na lesenihai ya Biashara –Aambatanishe kivuli cha leseni.
II. Mwombaji ni lazima awe na utambulisho wa mlipa kodi(TIN) – Aambatanishe kivuli cha utambulisho wa mlipa kodi(TIN namba au VAT)
III. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyo navyo, idadi ya wafanyakazi na uwezo wao.
IV. Mwombaje aonyeshe wazi wazi ofisi yake ilipo na uzoefu wa kazi anayoiomba.
V. Mwombaji asiwe mtumishi wa Halmashauri ya mji Kasulu.
VI. Atakayepata atatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya mji wa Kasulu.
VII. Mwombaji ajaze kiwango cha kodi atakacholipa kwa mwezi.
VIII. Bodi ya zabuni haitalazimika kukubali zabuni ambayo gharama zake ziko juu au chini sana. (atakayekidhi vigezo vya sharia ya manunuzi ndie atakaepewa kazi na Bodi ya zabuni.
IX. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo (kwa lakiri) juu ya bahasha ionyeshwe aina ya zabuni, namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo;-

**Katibu wa bodi ya zabuni,**
**Halmashauri ya mji wa Kasulu,**
**S.L.P 475, KASULU.**

Ada ya Zabuni hii ni Tsh.50,000/= na ilipwe kwa Mkurugenzi mtendaji Baada ya kupata namba ya malipo (control number) kutoka ofisi ya mapato iliyopo Halmashauri.

X. Kwa maelezo Zaidi kuhusiana na zabuni hii fika katika ofisi za Halmashauri ya mji Kasulu Muone katibu wa bodi ya zabuni.
XI. Vigezo vya tathimini ya zabuni zote nikama ilivyoainishwa kwenye tangazo pamoja na kwenye nyaraka za zabuni.
XII. Mwombaji wa mgahawa anatakiwa awe amesajiliwa na GPSA.

UTAWALA
Halmashauri Ya Mji
**KASULU**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
KASULU